

# CHUO KIKUU CHA SOKOINE CHA KILIMO

## CHAMA CHA WANATALUMA (SUASA)



## ZABUNI YA KUENDESHA SUASA CLUB

Chama cha wanataaluma wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUASA) kinakaribisha zabuni kutoka kwa watu wenye nia na uwezo wa kuendesha SUASA Club iliyoko Kampasi Kuu ya SUA.

### SIFA ZA MWOMBAJI

1. Awe na uthibitisho wa kutambuliwa kisheria na mamlaka husika
2. Awe na uthibitisho wa kuwa mlipa kodi mwaminifu
3. Awe na uzoefu unaothibitika wa kuendesha restaurant/ Mgahawa, bar au hotel
4. Awe na leseni hai ya kuendesha biashara husika

### MASHART YA ZABUNI

1. Mwombaji anatakiwa kununua nyaraka za zabuni zenye maelezo ya kina ya mahitaji ya zabuni hii iliyotangazwa kwa kulipa ada ya Tsh 50,000/= (Elfu Hamsini) taslimu kwenye akaunti namba 0152079421201-SUASA Benki ya CRDB, SUA fedha ambayo haitarejeshwa. Nyaraka zenye maelezo ya kina ya zabuni zinapatikana katika ofisi ya SUASA chumba namba 340/ 342 Kampasi Kuu, SUA. Nyaraka zitatolewa kwa aliyethibitisha kufanya malipo tajwa hapo juu.

2. Mwombaji anaruhusiwa kutembelea eneo la biashara yaani SUASA Club lililopo chuoni katika Kampasi Kuu siku za kazi kuanzia saa 2:00 asubuhi hadi saa 10:00 jioni. Mwombaji anashauriwa kuonana na uongozi wa SUASA ili kuona eneo husika Pia mwombaji anashauriwa kuwasiliana na wahusika; ambao namba zao zimeambatanishwa kwenye tangazo hili mara atakapohitaji maelezo mengineyo kuhusu zabuni hii.
3. Siku ya mwisho ya kuleta zabuni itakuwa tarehe 17 Machi, 2017 saa 8:00 Mchana. Maombi yatakayowasilishwa baada ya muda wa zabuni kuisha hayatapokelewa.
4. Zabuni zitafunguliwa mbele ya wazabuni wote walioomba au wawakilishi wao watakao amua kuhudhuria kwenye ufunguzi huo tarehe 20 Machi 2017 Saa 8:00 Mchana katika ukumbi wa Baraza la Chuo jengo la Utawala
5. Huduma inatakiwa kuanza kutolewa tarehe 01 Aprili 2017
6. Maombi ya zabuni yawekwe kwenye bahasha. Bahasha iandikwe “ ZABUNI YA KUENDESHA SUASA CLUB” na kufungwa kwa lakiri yatumwe kwa:

MWENYEKITI  
CHAMA CHA WANATALUMA  
CHUO KIKUU CHA SOKOINE CHA KILIMO  
S.L.P 3000  
MOROGORO

**Wasiliana kwa mwongozo Zaidi na:-**

1. Mwenyekiti SUASA-0752 562240
2. Katibu SUASA-0754477486
3. Mhazini SUASA 0655 441 788
4. Mwenyekiti kamati ya uendeshaji wa SUASA CLUB-0689 650 296